WITO WA MAOMBI YA

RUZUKU YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UTAWALA BORA, UJENZI WA AMANI NA UTATUZI WA MIGOGORO PAMOJA NA KUBORESHA MAISHA TANZANIA, 2019

Utangulizi

Foundation for Civil Society (FCS) ni shirika huru la kimaendeleo, la Kitanzania lisilolenga kupata faida, ambalo hutoa ruzuku na huduma za kuzijengea uwezo Asasi za Kiraia za Tanzania. Tangu kuanzishwa kwake FCS imechangia kwa kiwango kikubwa katika kuimarisha uwezo wa sekta ya kiraia nchini Tanzania. Kwa namna moja ama nyingine imeziwezesha asasi za kiraia kuwa na mchango unaoleta chachu ya maendeleo na kuhakikisha uwepo wa utoaji wa huduma bora zaidi, hasa katika ngazi za chini za jamii. FCS kupitia kazi za Asasi za Kiraia imeweza kuchangia uwepo wa hali bora ya maisha kwa Watanzania. Iwapo utapenda kupata taarifa zaidi kuhusu FCS, tembelea tovuti yetu: www.thefoundation.or.tz.

Wito huu wa maombi ya ruzuku unazihusu Asasi za kiraia za Kitanzania kutoka Tanzania Bara na Visiwani (Unguja na Pemba) kuomba ruzuku ili kutekeleza miradi katika Programu pana tatu kama ifuatavyo:- (i) Utawala Bora (ii) Ujenzi wa Amani na Utatuzi wa Migogoro na (iii) Kukuza Uchumi na kuboresha maisha.

1. PROGRAMU YA UTAWALA BORA

Wakati wa kuandaa Mpango Mkakati wake, FCS ilitambua na kutilia maanani ukweli kuwa Serikali ya Tanzania inafanya juhudi mahususi ili kuondoa umaskini kwa watanzania hasa walio wanyonge. Juhudi hizo ni pamoja na kuziba mianya ya rushwa na kupambana na matabaka ya walionacho na wasio nacho. Kadhalika, katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Tano, kiwango cha bajeti kinachopelekwa kuhudumia sekta nyeti kama Kilimo, Maji, Afya na Elimu kimeongezeka sana. Matarajio ya Serikali ni kwamba kwa kuongeza bajeti, huduma kwa wananchi wa hali ya chini itakuwa bora zaidi na hivyo kuwainua wanyonge toka katika kundi la umaskini. Hata hivyo, ili nia hiyo njema ya Serikali iweze kufikiwa ni lazima wananchi wahamasishwe kushiriki katika michakato mbalimbali ya maendeleo. Hii ni pamoja na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya maamuzi na kufanya kazi kwa karibu na Serikali zao za mitaa ili kuhakikisha fedha za umma zinatumika vizuri na kufikia malengo tarajiwa kwa faida ya walio wengi.

Matokeo I:

Viongozi wa serikali za mitaa wanatoa huduma bora zaidi kwa wananchi

Lengo kuu la matokeo tarajiwa ni kuhakikisha kuwa Serikali za Mitaa zinatoa huduma bora kwa wnanchi. Uwajibikaji na utoaji wa maamuzi unahitaji nguvu ya pamoja ya serikali na asasi zisizo za kiserikali ili kukuza/ kuongeza uwazi, uwajibikaji na matumizi ya utawala wa sheria kama vile maadili na uadilifu (kutokomeza rushwa) katika ngazi zote za serikali, sekta binafsi na vyama vya kiraia. Ushirikiano kati ya AZAKI na jamii utazihamasisha Serikali za Mitaa kuchapisha na kusambaza taarifa za mapato na matumizi kulingana na miongozo ya uwazi na uwajibikaji, vilevile kuheshimu na kuzingatia taratibu husika pamoja na utawala wa sheria. Hivyo basi FCS inatarajia kwamba, asasi za kiraia zitakuwa na uwezo wa kubuni miradi kwa ufanisi, itakayohakikisha kwamba jamii imehamasishwa, imewezeshwa na kuelimishwa jinsi ya kudai haki zao kwa mujibu wa sheria. Vile vile, viongozi wa serikali za mitaa watakuwa wasikivu zaidi kuhusu madai, mahitaji na kero za wananchi, hivyo kuanza kutumia mbinu shirikishi katika mikutano yote itakayofanywa kwa mujibu wa sheria, yenye lengo la kuhamasisha maendeleo ya wananchi.

Maombi yatakayotumwa eneo hili la matokeo yatahusu miradi inayohusiana na Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa Jamii (SAM) na Mfumo wa Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma (PETS). Hivyo, FCS inakaribisha maombi kutoka asasi za kiraia ambazo zitatekeleza miradi inayohusiana na:

a) Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa Jamii au Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma kwenye sekta ya elimu katika mikoa ya **Mtwara, Lindi, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Coast Region, Tanga, Singida, Rukwa, Kigoma, Geita, Mwanza, Katavi and Kagera pamoja na Unguja and Pemba.**
b) Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa Jamii au Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma katika sekta ya maji kwenye mikoa ya **Mtwara, Lindi, Singida, Dodoma, Simiyu, Geita, Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro, Mara na Tanga**

c) Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa Jamii au Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma kwenye sekta ya kilimo katika mikoa ya **Morogoro, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Songwe na Njombe.**
d) Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa Jamii au Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma kwenye sekta ya Afya katika mikoa ya **Katavi, Ruvuma, Njombe, Rukwa, Singida, Mbeya, Tabora and Tanga regions.**

Matokeo II:

Michakato ya maamuzi na ya kidemokrasia inahusisha makundi ya pembezoni (Watu Wenye Ulemavu, makabila madogomadogo Ethnic Minorities) na wanawake)

Serikali imefanya juhudi kubwa kupambana na mila kandamizi ikiwa ni pamoja na unyanyapaa kwa makundi maalumu wakiewemo watu wenye ulemavu. Hatua kadhaa zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kuandaa na kuzindua Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto unaolenga kushirikisha wadau wengine katika jitihada jumuishi za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto na hivyo kusaidia wahanga wa ukatili huo kupata huduma stahiki ili kudhibiti ukatili nchini. Hatua zingine ni kuanzisha Madawati ya Jinsia katika vituo mbalimbali vya Polisi kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi kwa wahanga wa ukatili. Kadhalika Serikali imedhamiria kuwezesha makundi maalumu wakiwemo watu wenye ulemavu, wanawake na vijana kwa kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha makundi hayo. Pamoja na juhudi hizo, changamoto za ukatili kwa makundi mbalimbali bado zipo zikiwemo suala la Ukeketaji, Ukatili kwa watoto (zikiwemo ubakaji, mimba za utotoni, ndoa za utotoni, pamoja na ukatili mwingine). Kadhalika ukatili kwa wanawake umekuwa ukiendelea ukihusisha ukatili wa kingono, kiuchumi ikiwemo kutopewa fursa ya kumiliki rasilimali muhimu kama ardhi na kadhalika. Watu wenye ulemavu wameendelea kupata changamoto kadhaa zikiwemo kutopewa fursa stahiki na kunyayapaliwa katika jamii. Bado kuna uelewa duni na kuaminika na kukubalika kuwa ulemavu wao siyo kigezo cha kushindwa kujihusisha na masuala ya kimaendeleo. Hivyo basi, chini ya matokeo haya, FCS itatoa fedha kwa asasi za kiraia ambazo mapendekezo yao ya miradi, miongoni mwa masuala mengine yataonesha kwamba:

- Makundi yaliyo pembezoni yanawezeshwa, yanapata huduma za kijamii tena yanashiriki kwa kujiamini katika michakato ya maamuzi.
- Wananchi wanadai haki zao tena wana ushawishi unaoleta mabadiliko.
- Wanawake wanaamini kwamba unyanyasaji wa kijinsia haukubaliki, tena wanaulaani, mila potofu zinakomeshwa, desturi zenye madhara zinasitishwa, sheria mbovu zinarekebishwa na wanawake wanaweza kupata, kumiliki na kufaidika na ardhi sambamba na mali nyingine.
- Maofisa wa serikali za mitaa na vyombo vya dola wanaitikia kwa wakati kuhusiana na mahitaji ya wanawake na makundi ya pembezoni.
- Watu wenye ulemavu wanatambuliwa na kujumuishwa kwenye ajenda na katika majukwaa muhimu ya maamuzi/ masuala ya watu wenye ulemavu yanazingatiwa na kujumuishwa katika ajenda na majukwaa ya maendeleo.
- Kupitishwa na kuingizwa kwa hatua na michakato maalum inayohusu mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu katika ngazi zote za serikali.
- Upatikanaji wa huduma bora za Elimu kwa watu wenye ulemavu
- Watu Wenye Ulemavu, wanawake, vijana na makundi ya makabila madogomadogo daima wanalindwa, wanatetewa, tena wanafurahia haki zao.

Kwenye eneo hili, FCS inakaribisha maombi kutoka kweye Asasi za Kiraia ambazo zitatekeleza miradi kwenye maeneo yafuatayo:

a) Utetezi na kupinga mila potofu kama Ukeketaji, Ukatili kwa wanawake na watoto (ikiwemo ubakaji, mimba za utotoni, ndoa za utotoni, pamoja na ukatili mwingine kwa wanawake. Mikoa lengwa ni **Mara, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Geita, Singida, Dodoma, Katavi, Rukwa pamoja na mikoa ya Unguja na Pemba.**
b) Utetezi kwa Watu Wenye Ulemavu ili kuongeza ushiriki wao kwenye michakato ya uwajibikaji kwa umma na serikali za mitaa, ambayo ni mahsusi kwa Mashirika na Mitandao ya Watu Wenye Ulemavu kutoka **mikoa yote ya Tanzania bara na Visiwani**.
c) Kukuza upatikanaji wa ardhi na haki nyingine za kumiliki mali, hasa kwa wanawake. Mikoa lengwa ni **Arusha, Manyara, Morogoro, Iringa na Mikoa iliyopo Unguja na Pemba**

2. PROGRAMU YA KUBORESHA MAISHA/ KUKUZA UCHUMI

Chini ya programu ya kuboresha maisha na kukuza uchumi FCS itawezesha miradi ambayo italenga kufikia matokeo yafuatayo:-

Matokeo 1:

Vijana (Wake kwa Waume) wajasiriamali wamepata masoko ya bidhaa zao na rasilimali za kujikimu kimaisha

Ukosefu wa ajira kwa vijana ni changamoto inayozikumba nchi nyingi duniani na ikiwemo Tanzania. Pamoja na uchuni wa Tanzania kukua kwa kasi kwa takriban muongo mmoja uliopita, bado changamoto za ajira hasa kwa vijana hazijaweza kutatuliwa kikamilifu. Kadhalika vijana wengi bado wana hama toka vijijini kuja mijini kwa lengo la kujitafutia kipato. Ili kuchangia katika utatuzi wa changamoto hizo, FCS itawezesha miradi ya kuboresha maisha na kukuza uchumi kwa vijana hasa katika Majiji ambako vijana wengi ndiko wanakokimbilia ili kupata fursa mbalimbali za kipato. Miradi itayofadhiliwa kwa upana ni ile itakayolenga kuwezesha yafuatayo:-

- Kuwezesha vijana kupata masoko ya bidhaa zao (Kuhamasisha Serikali za Mitaa kutenga maeneo ya masoko kwa vijana)
- Kuwezesha vijana kukuza mitaji ya biashara na kuboresha maisha yao
- Kuwezesha vijana kuanzisha miradi ya mtu mmoja mmoja au vikundi kwa ajili ya kuboresha maisha yao
- Kuhamasisha serikali za mitaa kuwawezesha vijana kupata 4% ya fedha zilizotengwa
- Kuhamasisha serikali za mitaa kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kukuza biashara zao/ kuboresha maisha.
- Kuhamasisha serikali za mitaa kuwawezesha vijana kupata nyadhifa mbalimbali kwenye vyombo vya maamuzi

FCS inakaribisha mashirika na Taasisi zinazoongozwa na vijana kutoka mikoa ifuatayo kuomba ruzuku kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Mikoa lengwa ni: **Arusha, Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Dodoma, Mwanza, Manyara, Morogoro, Iringa, Unguja na Pemba**

3. PROGRAMU YA UJENZI WA AMANI NA UTATUZI WA MIGOGORO

Pamoja na changamoto kadhaa katika ukanda huu wa Afrika, Tanzania imeendelea kuwa ni kisiwa cha amani ambapo dhana ya umoja na udugu zimeendelea kudumishwa. Hata hivyo, pamekuwa na viashiria kadhaa vinavyotokana na sababu mbalimbali ikiwemo ushindani wa kisiasa, ushindani juu ya umiliki wa rasilimali na kadhalika. Ili kuendelea kudumisha udugu na mshikamano kama Taifa FCS inazialika asasi za kiraia zenye utaalam wa masuala ya ujenzi wa amani na utatuzi wa migogoro kutoka (Tanzania Bara na Zanzibar – Unguja na Pemba) ambazo zina taaluma na uwezo wa kufanya kazi katika eneo hili kuomba ruzuku kutekeleza miradi ya Ujenzi wa Amani na Utatuzi wa Migogoro.

Lengo kuu: Kuchangia katika kukuza udugu na mshikamano katika jamii na makundi mbalimbali ya watu.

Asasi ambazo zimewahi kutekeleza miradi ya ujenzi wa Amani na utatuzi wa migogoro zinashauriwa kuangalia maeneo ya kuimarisha/ kuboresha katika miundo iliyotumika wakati wa utekelezaji wa mradi badala ya kuanzisha miundo mipya.
Kwenye eneo hili FCS inakaribisha maombi kutoka kwenye Asasi za Kiraia ambazo zitatekeleza miradi kwenye maeneo yafuatayo;

- Rasilimali hasa ardhi (Mikoa lengwa ni **Dodoma, Morogoro, Manyara and Arusha)**
- Migogoro ya Kisiasa (Kujenga Udugu katika jamii na vyama kati ya vyama mbalimbali vya Siasa – **Ngazi ya Taifa**)
- Migogoro kidini (Kujenga Udugu kati ya Dini mbalimbali- **Ngazi ya Taifa**)

4. Fursa ya Ruzuku kwenye wito huu wa maombi

Wito huu wa maombi ni kwa waombao ruzuku za ubunifu na ruzuku za kati. Maelezo ya kila fursa yameainishwa hapo chini:

Dirisha 1: Ruzuku za ubunifu. Ukubwa wa ruzuku unaanzia shilingi za Tanzania 20,000,000 hadi shilingi za Tanzania 49,999,999 kwa mwaka mmoja tu.

Ruzuku za ubunifu zinalenga asasi ambazo zitatekeleza ubunifu wao wenyewe dhidi ya changamoto zinazoikabili jamii. Kipindi cha utekelezaji wa mradi kitakuwa mwaka mmoja. Asasi itaweza kuomba kati ya shilingi 20,000,000 hadi shilingi 49,999,999. Asasi zinazolengwa na dirisha hili ni kubwa na ndogo, lakini zile ambazo zitakuwa na ubunifu wa kipekee wa kuzisaidia jamii zao kwa kuzingatia maelezo ya matokeo kama ilivyoelezwa hapo juu. Ruzuku bunifu kwa maana kwamba **Ubunifu kwa namna mradi umeundwa**, **ubunifu katika mkakati wa kutekekeleza unaopendekezwa, kwa ufanisi na kwa gharama ndogo za mradi** ili kufikia matokeo ya lengo. Dirisha hili pia linatoa mwanya kwa asasi ndogo, mpya na zenye mawazo chanya ya kutatua changamoto za kiutawala kwenye maeneo yao kupata ruzuku kutoka FCS. Hivyo, chini ya dirisha hili, FCS inakaribisha mapendekezo kutoka asasi za kiraia nchini kote ya kutekeleza miradi ya ubunifu / fikra, inayohusu programu ya utawala bora na programu ya kuboresha maisha/ Kukuza uchumi kama ilivyofafanuliwa na maeneo ya matokeo yaliyoainishwa hapo juu.

Dirisha 2: Ruzuku za Kati: Ukubwa wa ruzuku ni kati ya shilingi za Tanzania 50,000,000 hadi 120,000,000 kwa mwaka 1, kwa kipindi cha miaka 2 ya utekelezaji

FCS itatoa ruzuku ya ukubwa wa kati kwa AZAKi ili kutekeleza miradi kwenye maeneo ya matokeo yaliyoainishwa hapo juu. Kipindi cha utekelezaji wa mradi kitakuwa cha mwaka mmoja kwa kiasi kinachoanzia shilingi 50,000,000 hadi shilingi 120,000,000. Hata hivyo mwombaji anaweza kuomba hadi upeo wa shilingi 240,000,000 kwa kipindi cha miaka miwili kama maeneo tajwa hapo juu.

Kwa Azaki ambazo hivi sasa zina mikataba ya ruzuku na FCS, na shughuli zao zinaangukia kwenye maeneo ya wito wa sasa wa ufadhili, zinashauriwa kuboresha mapendekezo ya awali ili yaendane na wakati, zikizingatia mambo waliyojifunza wakati wa utekelezaji; na mabadiliko ya mazingira yaliyotokea katika kipindi cha utekelezaji, kisha kuwasilisha tena mapendekezo kamili yakiwa mwendelezo wa mipango ya mwaka 2019. Tafadhali onyesha wazi kwenye fomu ya maombi kwa kuangalia sanduku sahihi, mathalani, la wanaofadhiliwa hivi sasa. Zingatia kwamba waombaji wote wa ruzuku watapitia mchakato uleule kabla ya ruzuku kuidhinishwa.

****

5. MASUALA MUHIMU KWA WAOMBAJI WOTE

a) Katika kutoa ruzuku, FCS itatoa kipaumbele kwa Taasisi zinazoomba kutekeleza miradi katika Mikoa na Wilaya ambako zipo. Mfano, Kama Taasisi iko Wilaya ya Kasulu basi iombe kutekeleza miradi katika Wilaya hiyo au Wilaya zilizo jirani. Ni mara chache sana FCS itaweza kupitisha ruzuku kwa asasi ili kutekeleza mradi nje ya mkoa ilipo.

b) Chini ya wito huu wa maombi, asasi itaweza kutuma maombi ya mapendekezo ya mradi kwenye aina moja tu ya dirisha. Kwa kufafanua zaidi, ni kwamba iwapo asasi itaomba kwenye dirisha la pili - la Ruzuku za Kati, Asasi hiyohiyo haiwezi kutuma maombi kwa kupitia dirisha jingine la Ruzuku za Ubunifu au kinyume chake. Kadhalika Asasi itaruhusiwa kuomba aina moja tu ya Matokeo na Programu – Mfano- Taasisi itakayoamua kuomba Programmu ya Utawala Bora haiwezi kuomba tena programu zingine. Hivyo, Azaki zinashauriwa kuchagua dirisha na programu inalowafaa zaidi kulingana na malengo ya Taasisi na uwezo wao.

c) Wito huu wa maombi ya mapendekezo ya miradi ni kwa asasi za kiraia zilizosajiliwa, ambazo zinaendesha shughuli zake ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mashirika ya Kimataifa au maombi yoyote kutoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayatapokelewa.

(c) Foundation for Civil Society, ni asasi ya kiraia inayojitegemea kimamlaka. Tunayo sera ya kuendesha shughuli zetu zote kwa uaminifu na kimaadili. Katu hatuvumilii hongo na rushwa, kwani tumejikita kuendesha shughuli zetu na mahusiano yote kitaalamu, kwa haki, na uadilifu. Kwa hiyo tunawasihi waombaji wote kufuata utaratibu uliowekwa wa kupata ruzuku kutoka FCS, kwa kutumia daima njia sahihi za mawasiliano. Kwa kuwasiliana nasi, piga simu kupitia nambari+255 22 266 4890-2, simu ya mkononi +255 754 005708 au barua pepe: information@thefoundation-tz.org .

6. KANUNI ZA JUMLA ZA UPITISHAJI WA MIRADI

Kanuni inayoongoza uteuzi wa mradi wowote unaopewa ruzuku ni kwamba hatua zinazotegemewa kuchukuliwa na mradi shurti zilete manufaa yanayoonekana kwa wananchi wa maeneo yaliyochaguliwa ya hapa nchini.

Kanuni nyingine mahsusi zaidi, ambazo zitaoongoza uteuzi wa mradi, ni pamoja na:

a) Mashirika yaliyosalijiwa na kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria
b) Mashirika yenye mifumo thabiti ya utawala na utaratibu imara wa usimamizi wa fedha.
c) Kiwango ambacho shughuli za mradi uliopendekezwa zinaendana na Mpango Mkakati wa FCS na vipaumbele vyake.
d) Kiwango ambacho hatua za mradi zaweza kupimika na kuchangia kwenye matokeo tarajiwa
e) Jinsi na namna asasi itakavyohusisha jamii; mathalani uwakilishi, kiwango cha kuhusika kwa jamii pamoja na kueleweka kwa mradi, maendeleo na utekelezaji wake.

(e) Kiwango ambacho mradi unalitatua tatizo kwenye mazingira/ mahali kwa kuthibitishwa na ushahidi/ takwimu za uhakika.

(f) Uzingatiaji wa kuambatanisha nyaraka zote zinazoendana na maombi kama ilivyoainishwa kwenye fomu ya maombi.

Angalia: Orodha ya viambatanisho imo kwenye Fomu ya Maombi ya Mwaka 2019.

7. NANI ANAYETAKIWA KUTUMA MAOMBI

Taasisi zifuatazo zina sifa za kuomba ruzuku kutoka FCS:

1. Asasi za kiraia.
2. Mashirika yaliyojikita kwenye jamii (CBOs)
3. Mashirika ya Wataalamu
4. Vyama vya wafanyakazi
5. Vyombo vya habari
6. Taasisi za kidini[1]
7. Vyama vya ushirika[2]

8. YALE AMBAYO HATUTAYADHAMINI

FCS yaweza kutoa ruzuku kwa mashirika ya ndani, ambayo ni imara, tena hayakuanzishwa kwa madhumuni ya kupata faida binafsi. Hata kama shughuli ambayo umeiombea ruzuku ni ya kufanya hisani, haitakuwezesha kustahili kupata ruzuku, isipokuwa kama katiba ya taasisi yako inaelezea wazi aina ya hisani iliyosababisha kuanzishwa kwake. Iwapo unadhani kwamba asasi yako yaweza kuathirika na masharti haya, tafadhali tafuta ushauri kutoka FCS kabla ya kufanya maombi.

FCS haitatoa ruzuku kwa/kwa ajili ya:

1 Makanisa na misikiti si sehemu ya Asasi za Kiraia. Hata hivyo, FCS yaweza kutoa ruzuku kwa Taasisi za Kidini ambazo shughuli zake hazielekezwi kwenye kutangaza imani/ uinjilishaji.

2 FCS yaweza kutoa ruzuku kwa vyama vya ushirika ilimradi ruzuku itakayotolewa haitachangia kwenye faida, gharama au kupunguza madeni bali kwenye shughuli iliyolenga manufaa ya umma.

- Ufadhili & Udhamini.
- Miradi au shughuli zilizopo nje ya Tanzania.
- Miradi au shughuli ambazo zimeshakamilika
- Miradi inayotoa ruzuku kwa mashirika mengine
- Malipo ya ziada kwa wafanyakazi wa shirika wanaolipwa mshahara
- Ukuzaji wa kipato kwa asasi ndogondogo za kifedha
- Maombi kutoka kwa wataalamu wa kuchangisha pesa au washauri wa kitaalamu wanaofanya kazi kwa niaba ya mashirika
- Watu binafsi
- Vyama vya siasa
- Miradi inayopigia debe dini fulani, kabila au watu wa rangi fulani
- Biashara za sekta binafsi (ilimradi ziwe zisizokusudia kutengeneza faida)
- Mashirika ambayo yana madeni makubwa
- Waendesha Semina, warsha, na mikutano tu, isipokuwa kama ni sehemu ya shughuli zilizounganishwa na tokeo/mradi mahususi.
- Semina, labda zile ambazo ni sehemu ya shughuli pana zaidi, ambazo zinaunganishwa na matokeo dhahiri
- Gharama zisizotegemewa (dharura).
- Maombi ya Ruzuku Mkakati ili kutekeleza miradi ya Ukimwi.

9. TAREHE YA MWISHO YA KUTUMA MAOMBI

Maombi yote yaliyofanyiwa tafakari ya kina na mapendekezo ya miradi yaliyoandikwa vema yanatakiwa yatumwe na kumfikia **Mkurugenzi Mtendaji kabla ya saa 10.00 jioni mnamo tarehe 15 Januari 2019**. Mapendekezo ya mradi yatakayotumwa baada ya tarehe ya mwisho ya kutuma maombi hayatafikiriwa kwa ajili ya kupewa ruzuku na FCS.

10. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Katika wito huu, zipo njia mbili za kutuma maombi, moja ni kwa njia ya rejesta; mbili, kwa njia ya mkono. FCS haitapokea maombi yoyote yale yatakayotumwa kwa njia ya barua pepe au mtandao. ASASI inatakiwa kupakua fomu na viambatanisho vyake kutoka kwenye tovuti ya FCS http://www.thefoundation.or.tz. Tafadhali tumia fomu sahihi zitakazokuwepo kwenye tovuti na sio vinginevyo.

Maombi kamili ya Miradi yatatumwa kama nakala halisi (hard copy) yapelekwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji
The Foundation for Civil Society
7 Madai Crescent, Ada Estate Plot No. 154
P. O. Box 7192
Dar es Salaam
Simu ya Mezani +255 22 266 4890-2
Simu ya Mkononi: +255 754 005708
Tovuti: www.thefoundation.or.tz